JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1575,
Simu: (026) 2700157
Nukushi: (026) 2703014
Barua pepe: rbciringa@pccb.go.tz
Mtandao : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

JUNI 04,2020

TAKUKURU YAWAFIKISHWA MAHAKAMANI WALIOJIPATIA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI 500 KWA NJIA YA UDANGANYIFU

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, inatarajia kufungua mashtaka nane kwa kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa **wanane** kwa makosa 480 ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 577,670,428/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Watuhumiwa watakaofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa ni:

1. **JAMES JOSEPH MPILUKA (37)** ambaye ni Mfamasia.
2. **FAHAMU MAXIMILIAN KASAVAGA (46)** ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Klerruu
3. **DEOGRATIUS NAZARETH MWAILENGE (38)** Mfamasia
4. **GOODLUCK IDD MDUGI (39)** Mfamasia
5. **SABATHO LAZARO MUKAMA (39)** Mhadhiri chuo cha Uhasibu Arusha
6. **JULIUS KEHENGU JOSEPHAT (32)** Mteknolojia Maabara Halmashauri ya Manispaa Iringa

7. **FARIDA ISSA ALLY (32)** Mteknolojia Maabara (Kituo cha afya Ngome) Halmashauri ya Manispaa Iringa **pamoja na**
8. **EMMANUEL DONART MWANISENGA (32)** mwajiriwa wa Taasisi ya afya (PHCI), Iringa

(I) JAMES JOSEPH MPILUKA (37) ambaye ni Mfamasia, Yeye anatuhumiwa kwa makosa 59 ya utambulisho wa uongo kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 43,571,500/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Iringa ulibaini kwamba, Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi Oktoba, 2014 hadi Agosti mwezi Agosti, 2019 kwa kulipwa mshahara na stahiki zingine kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU huku akiwa tayari ameajiriwa na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.
Uchunguzi ulibaini pia kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya Mkataba wa Kudumu wa miaka mitatu RUCU tangu mwaka 2012 na baada ya kupata ajira ya kudumu Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto hakusitisha mkataba wake na RUCU bali aliendelea kusaini mkataba na kupata mshahara na stahili zote huku akifanya kazi sehemu zote mbili kwa mikataba ya kudumu huku akijua kwamba kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

Vile vile, tutamfikisha Mahakamani **(ii) FAHAMU MAXIMILIAN KASAVAGA (46)** ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Klerruu kwa makosa 87 ya utambulisho wa uongo kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya. Shilingi 146,607,240/= kama mshahara na shilingi 20,215,944/= stahiki zingine kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Iringa umebaini kwamba Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi Oktoba, 2012 hadi mwezi Disemba, 2019 kwa kulipwa mshahara na stahiki zingine kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU huku akiwa tayari ameajiriwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika kituo cha Kleruu Shule ya Sekondari tangu tarehe 01 Julai, 2002.

Uchunguzi ulibaini pia kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya mkataba wa kudumu wa miaka mitatu - mitatu RUCU tangu mwaka 2012 na huku akiwa na ajira ya kudumu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, aliendelea kusaini mkataba na kupata mshahara na stahili zote akifanya kazi sehemu zote mbili kwa mikataba ya kudumu huku akijua kwamba kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

Ndugu wanahabari,

Watuhumiwa wafuatao pia watawafikishwa mahakamani ambao ni: **(III) DEOGRATIUS NAZARETH MWAILENGE (38)** Mfamasia atafikishwa mahakamani kwa makosa 73 ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 117,078,048/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi Agosti, 2012 hadi mwezi Septemba, 2018 kwa kulipwa mshahara na stahiki zingine kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU bila kusema kama ni mwajiriwa wa kudumu TAMISEMI.

Uchunguzi ulibaini kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya mkataba wa kudumu wa miaka mitatu mitatu RUCU tangu mwaka 2012 na huku akijua anatenda kosa alisaini mkataba wake na RUCU na aliendelea kusaini mikataba na kupata mshahara na stahili zote akifanya kazi sehemu zote mbili kwa mikataba ya kudumu huku akijua ni kinyume cha sheria.

TAKUKURU Mkoa wa Iringa itamfikisha Mahakamani **(IV) GOODLUCK IDD MDUGI (39)** Mfamasia wa Manispaa ya Iringa kwa makosa 46 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 66,662,000/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi Octoba, 2015 hadi mwezi Julai, 2019 kwa kulipwa mshahara na stahiki zingine kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU bila kusema kama ni mwajiriwa wa kudumu wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa tangu mwaka 2014.

Uchunguzi ulibaini kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya mkataba wa kudumu wa miaka mitatu mitatu RUCU tangu mwaka 2015, huku akijua anatenda kosa, Aidha aliendelea kusaini mikataba na kupata mshahara na stahili zote kwa kufanya kazi sehemu zote mbili kwa mikataba ya kudumu huku akijua ni kinyume cha sheria.

Mtuhumiwa mwingine ni **(V) SABATHO LAZARO MUKAMA (39)** Mhadhiri chuo cha Uhasibu Arusha atafikishwa mahakamani kwa makosa 4 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 7,582,080/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi, Februari, 2015 hadi mwezi Agosti, 2019 kwa kulipwa mshahara kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU bila kusema kama ni mwajiriwa wa kudumu wa Chuo cha Uhasibu Arusha kuanzia Novemba, 2018 hadi Februari, 2019 aliendelea kupokea mshahara RUCU.

Uchunguzi ulibaini kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya mkataba wa kudumu wa miaka mitatu mitatu RUCU tangu mwaka 2015 hadi 2019 na akiwa ni mwajiriwa wa Chuo cha Uhasibu Arusha huku akijua anatenda kosa kwa kufanya kazi sehemu zote mbili.

Ndugu wanahabari,

(VI) JULIUS KEHENGU JOSEPHAT (32) Mteknolojia Maabara Halmashauri ya Manispaa Iringa ataungana na watuhumiwa wenzie kufikishwa mahakamani kwa makosa 55 ya kujipatia fedha njia ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 72,548,400/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwaka Machi 2015 hadi Julai 2019 kwa kulipwa mshahara kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU bila kusema kama ni mwajiriwa wa kudumu wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuanzia Novemba 2018 hadi Februari 2019. Aidha aliendelea kupokea mshahara RUCU.

Uchunguzi ulibaini kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya mkataba wa kudumu wa miaka mitatu mitatu RUCU tangu mwaka 2015 hadi 2019 na akiwa ni mwajiriwa wa Manispaa ya Iringa tangu 2015, huku akijua anatenda kosa kwa kufanya kazi sehemu zote mbili.

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Iringa inatarajia kumfikishwa Mahakamani **(VII) FARIDA ISSA ALLY (32)** Mteknolojia Maabara (Kituo cha afya Ngome) Halmashauri ya Manispaa Iringa kwa makosa 53 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh. 37,045,520/= kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi April 2015 hadi Julai, 2019 kwa kulipwa mshahara kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU bila kusema kama ni mwajiriwa wa kudumu wa Manispaa ya Iringa tangu mwaka 2015, huku akijua anatenda kosa kwa kufanya kazi sehemu zote mbili.

Aidha, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatarajia kumfikishwa Mahakamani **(VIII) EMMANUEL DONART MWANISENGA (32)** mwajiriwa wa Taasisi ya afya (PHCI), Iringa kwa makosa 103 ya kujipatia fedha njia ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu na kujipatia jumla ya Sh.85,575,640/= mishahara 74,721,360/= na Tsh. 10,854,280/= stahiki zingine kutoka Ruaha Catholic University (RUCU).

Mtuhumiwa aliyatenda makosa hayo kuanzia mwezi Februari, 2015 hadi Agosti 2019 kwa kulipwa mshahara na stahili zingine kama mwajiriwa wa kudumu wa RUCU bila kusema kama ni mwajiriwa wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto tangu Novemba 2017.

Uchunguzi ulibaini kuwa mtuhumiwa alikuwa akifanya kazi ya mkataba wa kudumu wa miaka mitatu mitatu RUCU tangu mwaka 2015 hadi 2019 huku akijua anatenda kosa kwa kufanya kazi sehemu zote mbili.

Ndugu wanahabari,

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatoa wito kwa watumishi wa Umma mkoani humu ambao wanajihusisha na vitendo vya uvunjifu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, kuacha vitendo hivyo mara moja kwa kujiepusha na mgongano wa maslahi na Mwajiri na ukikaji wa Maadili ya Umma. Aidha Waajiri wanawajibika kufuatilia vitendo hivyo na kuchukua hatua kama ilivyoainishwa kwenye Sheria na kanuni za kudumu za utumishi wa umma.

Imetolewa na:

SGN
Mweli E. Kilimali,
Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa